

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

**TANGAZO KWA UMMA KUHSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu, ambapo jumla ya **Shilingi 765,317,900** zimetengwa katika robo ya 1 ya mwaka wa fedha 2024/2025 Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenyewe ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyewe ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha

- kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyenye akili timamu na wenyenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa na wanakundi wenyenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;

- i. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji.
- ii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo,
- iii. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyondani ya mfumo.
- iv. Taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 31 Oktoba Mwaka 2024

Tangazo hili limetolewa na: -


Mkurugenzi Mtendaji Wilaya

Halmashauri ya Wilaya

UYUI

